**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**

# TANGAZO

## FURSA YA KUJIUNGA NA PROGRAMU YA BBT

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa inawatangazia nafasi za kujiunga na program ya Jenga Kesho Bora (Building a Better Tomorrow-BBT) itakayotoa mikopo yenye riba nafuu zaidi katika sekta ya kilimo, hivyo anakaribisha maombi kwa vijana na wanawake wote wa kitanzania wenye sifa kuleta maombi ya kujiunga na fursa hiyo.

**UTANGULIZI:**

Programu ya BBT inalenga kupunguza changamoto ya ajira na kuhamasisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo, maeneo ya mashamba, mitaji na kuwaunganisha na fursa za masoko.

Utekelezaji wa program hii unahusisha mashamba makubwa ya pamoja (Block Farms), huduma za ugani, uchimbaji wa visima vya umwagiliaji na mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake.

**MAENEO YATAKAYOGHARAMIWA NA MIKOPO KATIKA PROGRAMU HII;**

1. Kilimo cha mazao ya muda mfupi.
2. Miundombinu ya umwagiliaji (Visima, Mifumo Ya Umwagiliaji).
3. Uongezaji wa thamani wa mazao.
4. Pembejeo za kilimo (Mbegu, Mbolea, Viuatilifu).
5. Gharama za uendeshaji wa shamba (Kusafisha, Kulima, Kupanda n.k)
6. Uhifadhi wa mazao na vifungashio vya mazao.
7. Zana za kilimo kama trekta, trekta za mikono (Powertiller).

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania na wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.
ii. Mwombaji anatakiwa kuwa na umri kati ya miaka **18-40.**
iii. Awe tayari kujifunza na kushiriki shughuli za kilimo biashara.
iv. Awe tayari kujitolea na kujifunza ujasiriamali.
v. Awe anajua kusoma na kuandika mwenye elimu angalau ya shule ya msingi .
vi. Awe hajaajiriwa.
vii. Awe mwenye tabia njema.
viii. Awe anamiliki ardhi yenye ukubwa wa kati ya **ekari 1** hadi **ekari10** kisheria.
ix. Awe na Barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Serikali ya Kijiji/Mitaa.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

- Fomu za kujiunga zinapatikana katika ofisi za kata.
- Mwanamke mwenye umri zaidi ya miaka 40 anaruhusiwa kuomba.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na nyaraka za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- Mwisho wa kutuma maombi ya programu hii ni tarehe **2 Machi, 2026.**
- Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatashughulikiwa.
- Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya programu iliyosainiwa pamoja na barua ya utambulisho kutoka serikali ya Kijiji/Mitaa, Anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa,
Barabara ya Nyerere,
S.L.P. 90,
Mbamba Bay,
**57582 Nyasa – Ruvuma.**

**Tangazo hili linapatikana pia katika tovuti ya Halmashauri, *(www.nyasadc.go.tz)***

Tangazo hili limetolewa na:

Khalid A. Khalif
**MKURUGENZI MTENDAJI**

**22 Januari, 2026**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
P. O. Box 90, MBAMBA BAY
NYASA DISTRICT COUNCIL